



## KITUO CHA WAFANYAKAZI CHA WNYCOSH FAHAMU HAKI ZAKO

### Kima cha Chini cha Mshahara

**\$14.20/saa**

Vibarua wa mashamba wana kima cha chini cha mshahara cha \$14.20/saa, na “mikataba ya wafanyakazi wa mashamba” inayobainisha jinsi mapato yanavyochumwa na hali ya mazingira ya kazi

### Ratiba ya Vima vya Chini vya Mishahara\*

Mwaka	Kima cha Chini cha Mshahara/saa
2024	\$15.10
2025	\$15.75

\*Nje ya Mji wa New York

### Wafanyakazi Wanaopewa Bahshishi

- Mapato ya \$9.45/saa na kiwango cha chini cha malipo cha \$4.75 kinachotolewa kama bahshishi **AU** kulipwa na mwajiri
- Kiwango cha bahshishi anachofaa kupata mfanyakazi au kinacholipwa na mwajiri huongezeka kulingana na kima cha chini cha mshahara
- Wafanyakazi wanaopewa bahshishi wako chini ya masharti ya ovataimu
- Wafanyakazi wanaopokea bahshishi au kiinua mgongo **huenda bahshishi zao zisidaiwe au kutiliwa mkazo kwa njia ya moja kwa moja au mbadala na mwajiri ua kwa niaba ya mwajiri**

### Haki za Wafanyakazi wa Muda

Wafanyakazi wa muda wana haki ya:

- Kutobaguliwa na **wakala** wanaotumia na PIA mwajiri mwenyeji
- Kupokea mafundisho sawa au yanayolingana kuhusu usalama na wafanyakazi wa kudumu wa mwajiri
- Kima cha chini cha mshahara

### Haki ya Mazingira Salama na yenye Afya

Chini ya sheria za afya na usalama za Marekani, una haki ya:

- Kufundishwa katika lugha unayoelewa
- Kuwa katika mazingira ya kazi yaliyo salama na yasiyo na hatari zinazotambulika
- Kupiga ripoti kwa msimamizi wako iwapo una shaka kuhusu afya na usalama
- Kuwasilisha malalamishi kwa OSHA kuhusu mazingira yasiyokuwa na usalama au afya njema
- Kukataa kufanya kazi unayodhania kwamba itakuweka kwenye hatari mara moja
- Kufahamu hatari zilizo katika mahali pa kazi
- Kutobaguliwa (kufutwa, kupewa kazi mbaya zaidi, n.k.) kwa kupiga ripoti kuhusu hali za hatari kwa usalama (Ulinzi kwa Watoa Taarifa)
- Kuweza kupata rekodi za vipimo vya afya na vipimo vya uchunguzi wa kuwepo kwa vifaa hatari katika mazingira ya kazi
- Kupata habari kuhusu visa vya majeraha au magonjwa vinavyotokea kazini

## Ovataimu

Wafanyakazi wengi wanastahili kupata mara 1 ½ ya malipo yako ya kawaidakwa kila saa baada ya kuhudumu masaa 40 katika wiki

Masharti ya ovataimu huenda yasitumike kwa:

- Vibarua wa Mashamba
- Wafanyakazi Watendaji: wanaoweza kuajiri/kufuta na wanaoelekeza shughuli za kazi za wafanyakazi wawili au zaidi kwa mara nyingi
- Wafanyakazi Wataalamu: walio na digrii ya miaka 4 au ambao kazi zao ni za ubunifu
- Wafanyakazi Wasimamizi: wanaofanya maamuzi ya busara na huru au ambao kwa wakati mwingi hufanya kazi za ofisi/kazi za uwandani zisizo za mikono zinazohusiana moja kwa moja na sera za usimamizi

### Marudio ya Kupokea Malipo

Ni lazima wafanyakazi wengi wapate malipo ya kazi zao ndani ya siku 7 baada ya kipindi walichofanya kazi

### Haki ya Kutobaguliwa

Sheria ya Title VII na Kitengo cha Haki za Binadamu cha Jimbo la New York hulinda wafanyakazi kutokana na ubaguzi.

## Makundi Yanayolindwa Kutoka kwa Ubaguzi

- Asili
- Rangi
- Nchi ya Asili
- Dini
- Jinsi
- Ulemavu
- Utambulisho wa Hisia za Kimapenzi
- Hali ya Uanajeshi
- Hali za Kijeni Zinazobainisha Mielekeo
- Hali ya Familia
- Hali ya Ndoa
- Halia ya Kuathiriwa katika Vita vya Kinyumbani
- Ujauzito
- Shughuli za Kiasia (nje ya kazi)
- Shughuli za Kujiburudisha (nje ya kazi)
- Uanachama katika Miungano

## Ulinzi wa Watoa Taarifa

Ni hatia kumwadhibu au kumfuta mfanyakazi kwa kutoa au kuwasilisha malalamishi kwa wakala yeyote wa serikali

Mwajiri **hafai** kuwaadhibu wafanyakazi kwa kushtaki mwajiri kwa wakala wa serikali kwa nia njema

Mwajiri huenda akatakiwa kuwajibika kisheria iwapo atalipiza kisasi kwa:

- Kufuta/Kuachisha kazi
- Kuweka mwajiri kwenye orodha ya watu wabaya
- Kushusha cheo
- Kunyimwa malipo ya Ovataimu/ Kupandishwa Cheo
- Kukosa kuajiriwa/kuajiriwa tena
- Kutia woga
- Kutoa vitishoi
- Kupunguza Malipo
- Kupunguza Masaa ya Kazi
- Kuadhibu
- Kutotoa mafao
- Kuteua mfanyakazi kwa kazi nyingine kunakoathiri uwezekano wa kupandishwa cheo

## Haki ya Malipo kwa Wafanyakazi

Ukijeruhiwa ukiwa kazini:

- Una haki ya kuwa na bima ya mishahara ya wafanyakazi, hata ikiwa malipo yako si rasmi au hayarekodiwi
- Unafaa kujaza fomu ya madai ya Wafanyakazi au ya C-3 kupitia mwajiri wako au unaweza kupokea usaidizi kupitia Simu ya Moja kwa Moja ya Kituo cha Wafanyakazi cha WNYCOSH: **(716) 206-3550**